

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI  
JESHI LA POLISI TANZANIA**



**TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA**

Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania anatangaza nafasi za ajira kwa waliohitimu mafunzo ya kujenga Taifa (JKT) na Kujenga Uchumi (JKU), waliopo kwenye makambi na nje ya makambi wenye elimu ya Shahada, Stashahada, Astashahada, Kidato cha sita na Kidato cha nne.

**1. Sifa za Waombaji**

- a) Awe raia wa Tanzania kwa kuzaliwa.
- b) Awe amehitimu kidato cha nne au cha sita kuanzia mwaka 2017 hadi 2022.
- c) Kwa waombaji wa kidato cha nne na sita wawe na umri kuanzia miaka 18 hadi 25.
- d) Kwa waombaji wa kidato cha nne wawe na ufaulu wa daraja la kwanza mpaka la nne (Division I – IV). Kwa waombaji wenye ufaulu wa daraja la nne (Division IV) wawe na ufaulu wa alama (Point) 26 hadi 29.
- e) Kwa waombaji wa kidato cha sita wawe wamesoma masomo ya sayansi na ufaulu wa daraja la kwanza mpaka la tatu (Division I – III)
- f) Wahitimu wa Shahada, Stashahada na Astashahada wawe na umri kuanzia miaka 18 hadi 29.
- g) Awe na urefu usiopunguwa futi tano na inchi tano (5'5") kwa wanaume, na futi tano inchi mbili (5'2") kwa wanawake.
- h) Awe na kitambulisho cha taifa au namba ya utambulisho kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).
- i) Awe na afya njema kimwili na kiakili iliyothibitishwa na daktari wa Serikali.
- j) Awe hajaoa/kuolewa au kuwa na mtoto.
- k) Awe hajawahi kutumia madawa ya kulevya.
- l) Awe tayari kuhudhuria mafunzo ya awali ya taaluma ya Polisi.
- m) Awe hajaajiriwa au hajawahi kuajiriwa na taasisi nyingine ya Serikali.
- n) Awe tayari kufanya kazi za Polisi mahali popote Tanzania.
- o) Awe tayari kujigharamia katika hatua zote za usaili endapo ataitwa
- p) Asiwe na alama za kuchorwa mwilini (tattoo).
- q) Asiwe na kumbukumbu za uhalifu.
- r) Kwa waombaji wenye elimu ya kiwango cha Shahada (NTA level 8), Stashahada (NTA level 6) na Astashadaha (NTA Level 5 au NVA Level 3) wanatakiwa wawe na fani zilizoainishwa kwenye tangazo.

## **2. Utaratibu wa kutuma Maombi**

1. Waombaji wote wanatakiwa waandike barua za maombi wao wenyewe kwa mkono (Handwriting) bila kusahau namba za simu, na watumie anuani ya Mkuu wa Jeshi la Polisi S.L.P 961 DODOMA.
2. Waombaji wote waambatanishe nakala zifuatazo:
  - a) Nakala ya cheti cha kuzaliwa
  - b) Nakala ya kitambulisho cha Taifa cha NIDA au namba ya NIDA
  - c) Nakala ya cheti cha kuhitimu mafunzo ya JKT/JKU kwa walio nje ya makambi.
  - d) Nakala za vyeti vya taaluma (Academic Certificates).
  - e) Nakala za vyeti vya kuhitimu mafunzo ya sekondari (Leaving Certificate).
3. Kwa waombaji wa kidato cha sita na cha nne ambao wamehitimu mafunzo ya JKT/JKU waliopo nje ya makambi (urairani) maombi yao yapelekwe kwa Makamanda wa Polisi wa Mikoa waliopo na sio Makao Makuu ya Polisi Dodoma.
4. Kwa waombaji wa kidato cha sita na cha nne waliopo kwenye makambi ya JKT/JKU maombi yao yawasilishwe kwa Makamanda wa Polisi wa Mikoa kupitia kwa Wakuu wa Kambi.
5. Kwa waombaji wenye elimu ya Shahada, Stashahada na Astashahada zilizoainishwa kwenye tangazo hili wanatakiwa kupakua (download) na kujaza fomu maalum (Kiambatisho 'B') inayoonyesha taarifa zake binafsi. Fomu hiyo imeambatanishwa kwenye tangazo na inapatikana kwenye tovuti ya Polisi. Utumaji wa fomu hiyo uwe kwa njia ya 'excel' na usiwe kwa njia ya kuskani (pdf) isipokuwa barua za maombi na vyeti ndio viskaniwe (pdf). Kwa waombaji wa Tanzania Bara Maombi yatumwe kupitia barua pepe [admin.phq@tpf.go.tz](mailto:admin.phq@tpf.go.tz) na kwa waombaji wa Zanzibar yatumwe kupitia barua pepe [ajira.znz@tpf.go.tz](mailto:ajira.znz@tpf.go.tz). Maombi yatakayotumwa kwa mkono au kwa njia ya Posta hayatopokelewa.
6. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 16/10/2023.

Imetolewa na:

**Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania**

**Makao Makuu ya Jeshi la Polisi**

**S.L.P 961**

**DODOMA**

**09/10/2023**

<b>FANI ZINAZOTAKIWA KWA KILA NGAZI YA ELIMU</b>	
<b>SHAHADA</b>	
<b>S/NO</b>	<b>FANI</b>
1	Architectures
2	Arts in French, Portuguese, Chinese and Arabs
3	Arts in Linguistics
4	Automobile Engineering
5	Boat Building
6	Civil Structural Engineering
7	Cyber forensic and Cyber security
8	Dental officer
9	Disaster Management
10	Electromechanics
11	Fibre glass
12	Laboratory science
13	Law Enforcement (BALE)
14	Marine Engineering
15	Marine Transportation
16	Master Fisherman
17	Mechatronic Engineering
18	Medical Doctor
19	Motor Vehicle Mechanics
20	Navigation
21	Physiology
22	Physiotherapy
23	Psychology
24	Quantity Surveyors
25	Radar Operation
26	Radar Technician
27	Radiology
28	Taxation
29	Theatre and Performing arts
30	Translation and Interpretation
31	Truck Mechanics

<b>STASHAHADA</b>	
1	Architectures
2	Arts in French, Portuguese Chinese and Arabs
3	Aluminium Fitting and Fabrication
4	Automotive Air Condition
5	Electromechanics
6	Auto Electrical Engineering
7	Boat Building
8	Carpentry and Joinery
9	Cyber forensic and Cyber security
10	Electrical Engineering
11	Electrical installation and Industrial
12	Electronics and Telecommunication
13	Health Record management
14	Hotel management
15	Motor Cycle Mechanics
16	Motor Vehicle Mechanics
17	Navigation
18	Painting & Sign writing
19	Psychology
20	Radar Operation
21	Radar Technician
22	Refrigeration & Air Condition
23	Secretarial
24	Shipping and Logistic
25	Sound Engineering
26	Tailoring
27	Theatre and performing Arts
28	Truck Mechanics
29	Vehicle Programmer
<b>ASTASHAHADA</b>	
1	Agriculture and Livestock
2	Aluminium fittings & Fabrications
3	Auto electrical Technician
4	Automotive Air Condition Technician
5	Boat Skippers

6	Body repair and Spray painting
7	Carpentry & Joinery
8	Car Interior Design Technician
9	Computer Application
10	Driving (class E & D)
11	Electrical Installation and Industrial
12	Electrical Technician
13	Electromechanics
14	Fitting and Turner
15	Hotel management
16	Information and communication Technology
17	Leather crafting
18	Mandatory course certificate
19	Masonry and Bricklaying
20	Mechanical Engineering
21	Mechatronic Engineering
22	Medical Records
23	Motor Cycle Mechanics
24	Motor Rewinding
25	Motor vehicle mechanics
26	Music and Sound production
27	Navigation
28	Nursing
29	Painting and Sign writing
30	Panel Beating
31	Performing Arts
32	Photocopy and Printer Maintenance
33	Plumbing and Pipe fitting
34	Quality manager
35	Records and Archive management
36	Refrigeration and Air Condition
37	Rescue Boat
38	Safety Manager
39	Scuba diving
40	Secretarial
41	Sewing Machine Maintenance

42	Sign Language
43	Sports (Football, athletics, Volleyball, Basketball, Handball, Boxing, Judo, Karate and Swimming)
44	Tailoring
45	Truck Mechanics
46	Turning & fittings
47	Vehicle Programing
48	Welding & Fabrication